

Unapopanga miliki, mpangaji anakubali kuweka saini hati ya kukodisha kwa kipindi cha miezi 6 au miezi 12.

Kama ukichagua kuondoka mwisho wa kipindi cha mkataba wako wa kupangisha – lazima umpe ajenti au kabaila notisi ya siku 14 kwa maandishi.

Hakikisha kwamba ilani inawaeleza tarehe unayotaka kuhama miliki.

Tunza nakala ya barua, na andika makumbusho ya tarehe ulipoituma au kusalisha.

Je, inakuwaje kama ukitaka kuendelea kupanga miliki?

Baada ya mkataba kumaliza waweza kuweka saini kwa hati mpya ya kukodisha ukitaka kuendelea kupanga miliki – lakini si lazima.

Kama ukiweka saini kwa hati mpya ya kukodisha na unataka kuhama – lazima umpe ajenti au kabaila notisi ya siku 21.

Lazima ulipe kodi yako mpaka mkataba wako unapomaliza.

Je, inakuwaje ukihama kabla mkataba kumaliza?

Unavunja mapatano yako ya upangaji.

Umjulisha ajenti au kabaila mapema yawezakanavyo.

Labda utahitaji kuendelea kulipa kodi mpaka ajenti au kabaila anapata mpangaji mpya.

Pia wanaweza kukutoza kwa gharama ziada kupata mpangaji mpya – kwa mfano, kodi, matangazo na ada ya kukodisha tena.

Lakini kama mkataba wako una 'ada ya kuvunja' ndani ulipe kiasi hiki badala yake.

Lazima kabaila atende kutafuta mpangaji mpya mapema yawezakanavyo.

Wakati wengine waweza kumaliza mkataba wako mapema bila kulipa gharama ziada.

Kwa mfano:

- kama ukikubali nafasi ya nyumba ya jamii/serikali
- kama ukihamia nyumba ya wazee

- kama ukikuwa na Apprehended Violence Order (AVO) (Agizo la kushikwa ukifanya ujeuri) kupinga mtu ambaye anaishi katika miliki
- kama kabaila anataka kuuza miliki na hakukuambia ulipoweka saini kwa hati ya kukodisha.

Mkataba unaweza kumalizika wakati wowote kama kabaila na mpangaji wanakubali wote wawili

Je, jinsi unaweza kupata pesa zako za dhamana kurudishwa?

Ulilipa dhamana ya thamani sawa na kodi ya wiki 4 ulipoweka saini kwa hati ya kukodisha.

Upate pesa zote za dhamana kurudishwa kama ukiacha miliki katika hali sawa na hali yake ulipohamia – na huna deni yoyote kwa kabaila.

Ajenti au kabaila atafanya ukaguzi wa mwisho wa miliki baada ya umeshahama.

Taarifa ya hali itatumiwa kuangalia kwa madhara au kama kuna chochote kinachohitaji kusafishwa bado.

Wapangaji hawana majibu kwa madhara iliyosababishwa na matumizi ya kila siku, kwa mfano sehemu ya juu ya meza au zulia iliyochakavu.

Kama ukiacha miliki kuwa mchafu au kwa hali mbaya – labda hutapata pesa zote zako za dhamana.

Omba ajenti au kabila kujaza fomu ya Claim for refund of bond money na kusalisha na Fair Trading wewe mwenyewe.

Kama huweza kukubali na ajenti au kabaila yako, pata ushauri kutoka Tenants Advice and Advocacy Services (TAAS) (Huduma za Ushauri na Utetesi wa Wapangaji).

Au waweza kuomba kwa Tribunal kufanya uamuzi.

Kupata maelezo zaidi kuhusu haki na majukumu ya wapangaji, tembelea tovuti ya Fair Trading kwa www.fairtrading.nsw.gov.au au piga simu namba ya 13 32 20.

Kama ukihitaji msaada wa lugha pigia simu 13 14 50.